

**Ndugu Kaimu Mkurugenzi
Ofisi ya Makamu Rais
Ndugu Viongozi**

**RISALA
MABADALIKO YA MAJIRA**

Sisi, mashirika na watu binafsi nchini Tanzania, tuliosaini hapo chini, leo tarehe 8. 12. 2007, kwa pamoja tunashirikiana na mashirika na watu binafsi ulimwenguni kushinikiza kuchukuliwa hatua madhubuti dhidi ya mabadiliko ya majira.

Mabadiliko ya majira ni tatizo kubwa linalokikabili kizazi cha sasa. Ni tatizo la kitabaka na la ulinzi wa mazingira, kwa sababu linatishia maisha ya watu maskini na wale walio pembezoni. Watu katika nchi kama yetu, Tanzania, wana uwezo mdogo wa kukabiliana na athari zinazotokana na mabadaliko ya majira kama vile mafuriko, ukame, vimbunga n.k. Kilimo ndio chanzo kikuu cha chakula kinachotegemewa na asilimia 90 ya watanzania; kinakabiliwa sana na mabadiliko ya majira na mvua. Nchini mwetu hali ya maisha ya watu yapo hatarini kutokana na athari zitokanazo na mabadaliko ya majira. Kuyeyuka kwa barafu katika kilele cha mlima Kilimanjaro ni dalili ya wazi ya mabadiliko ya majira na hili haliwezi kufumbiwa macho na mtu yeyote. Magonjwa kama Malaria sasa yameenda hata sehemu ambazo hapo awali hayakuwepo.

Majira ya msimu ya Tanzania yameshaanza kubadilika - tunaweza kupata mafuriko mwezi Mei au ukame baada ya miaka mitatu. Vina vya maji vimepungua sana. Mvua zinanyesha wakati usio muafaka kwa wakulima na kusababisha matatizo mengi ikiwemo tatizo la njaa.

Nchi zilizoendelea kiviwanda, ambazo zinatoa mchango mkubwa wa hewa ya kabonidiyoksidi angani kwa miaka 200 tangu mapinduzi ya viwanda, ndizo zinatakiwa kuwajibika kwa tatizo hili na ndizo hasa zinatakiwa kuwajibika na upunguzaji wa utoaji wa carbon dioxide. Hata hivyo, Tanzania nayo inawajibika kuhakikisha kuwa kadiri iwezekanavyo inaendelea kupitia njia safi na sahihi ili kuleta maaendeleo endelevu.

Tunatoa wito wa **“kuungana na kushikamana”**. Mataifa yanayoendelea hayatakiwi kuzuiliwa katika jitihada zake za maendeleo na kupunguza umaskini. Nchi za kitajiri zinatakiwa kuwajibika na inatakiwa nchi zilizoendelea kiviwanda kuingia katika mikataba ya kupunguza utoaji wa carbon dioxide. Hata hivyo nchi zinazoendelea zinatakiwa kuongeza bidii kuendelea kwa njia safi na kuepuka matumizi ya teknolojia ya carbon dioxide, inapowezekana. Zinatakiwa kuungwa mkono na nchi zilizoendelea kiviwanda katika juhudi hizo.

Hii ina maana kwamba, pale inapowezekana, na bila kuzuia maendeleo ya nchi, Tanzania ihakikishe kuwa:

- Inatumia teknolojia safi kama vile nishati inayotokana na nguvu ya maji, jua, upepo na nguvu za mawimbi ya bahari katika sekta ya umeme
- Kupanda miti mingi hasa sehemu zinazokatwa miti kwa ajili ya mkaa
- Katika sekta ya usafiri zitumike injini safi na kuweke kipaumbele kwa usafiri wa umma na baisikeli
- Kuweka kipaumbele kwenye utafiti wa gesi asilia mafuta yatokanayo na mimea ambayo inaweza kulimwa nchini
- Kuhamasisha wafanyabiashara na wawekezaji kuzalisha kutumia teknolojia inayopunguza hewa chafu na moshi ya carbon dioxide
- Kutumia kwa usahihi fursa za ufadhili na kujenga uwezo wa maendeleo safi

Muda wa kuchukua hatua dhidi ya mabadiliko ya majira ni sasa.

- Centre for Energy Environment Science & Technology (CEEST)
- Envirocare
- Joint Environment and Development Management Action (JEMA) – University of Dar es Salaam
- Journalists Environmental Association of Tanzania (JET)
- Legal and Human Rights Centre (LHRC)
- Tanzania Association of NGOs (TANGO)
- Tanzania Coalition for Sustainable Development (TCSD)
- Tanzania Traditional Energy Development and Environmental Organization (TaTEDO)
- Tanzania Youth Environment Network (TAYEN)
- Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA)